**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora

# SERA YA UTAWALA BORA

**2011**

# YALIYOMO


UFUPISHO II
DIBAJI II
1 UTANGULIZI 2
1.1 UTANGULIZI 2
1.2 HAJA YA KUWA NA SERA YA UTAWALA BORA 2

2 MAANA NA MISINGI YA UTAWALA BORA 2
2.1 MAANA YA UTAWALA BORA 2
2.2 MISINGI YA UTAWALA BORA 2
2.2.1 Uwajibikaji na Uwazi 2
2.2.2 Utawala wa Sheria na Haki za Binadamu 2
2.2.3 Kuzuia rushwa 2
2.2.4 Ufanisi na tija 2
2.2.5 Ushirikishwaji 2
2.2.6 Kuzingatia matakwa ya wananchi 2

3 DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA 2
3.1 DIRA 2
3.2 DHAMIRA 2
3.3 LENGO KUU 2
3.3.1 Malengo mahususi 2

3.4 LENGO MAHUSUSI 1:
KUZIWEZESHA WIZARA, IDARA NA TAASISI
ZA SERIKALI NA JUMUIYA ZA KIRAIA KUFUATA
MISINGI YA UTAWALA BORA 2

3.5 LENGO MAHUSUSI 2: KUWEKA MIFUMO YA KUPIMA
VIWANGO VYA KUHESHIMU AU KUTEKELEZA MISINGI YA
UTAWALA BORA KATIKA NGAZI ZOTE 2

3.6 LENGO MAHUSUSI 3: KUFANYA MAPITIO YA
SHERIA NA MIUNDO YA TAASISI INAYOELEZEA
MAJUKUMU YA WIZARA, IDARA NA TAASISI ZA
SERIKALI. 2

3.7 LENGO MAHUSUSI 4: KUWEKA TARATIBU ZA KUIMARISHA URATIBU NA UTEKELEZAJI FANISI WA PROGRAMU ZA UTAWALA BORA 2

3.8 LENGO MAHUSUSI 5: KUHAKIKISHA KWAMBA HAKI YA KUPATA HABARI INATEKELEZWA KIKAMILIFU 2

3.9 LENGO MAHUSUSI 6: KUHAKIKISHA KWAMBA TATHMINI YA KINA YA UTAWALA BORA INAFANYIKA HAPA ZANZIBAR. 2

3.10 LENGO MAHUSUSI 7: KUWEKA MIFUMO MADHUBUTI YA KUZUIA RUSHWA 2

3.11 LENGO MAHUSUSI 8: KUJENGA TAASISI ZENYE UFANISI, TIJA NA SIKIVU 2

3.12 LENGO MAHUSUSI 9: KUIMARISHA SERIKALI ZA MITAA. 2

3.13 LENGO MAHUSUSI 10: KUIMARISHA TAASISI ZA UANGALIZI. 2

3.14 LENGO MAHUSUSI 11: KUIMARISHA UWAJIBIKAJI WA VIONGOZI WALIOCHAGULIWA KWA WANANCHI. 2

3.15 LENGO MAHUSUSI 12: KUHAKIKISHA UHESHIMU WA MAJUKUMU YA KIJAMII. 2

3.16 LENGO MAHUSUSI 13: KUWEKA MAZINGIRA WEZESHAJI, FANISI NA YA KIMUONGOZO KUHUSU UTAWALA BORA KIBIASHARA 2

3.17 LENGO MAHUSUSI 14: KUIMAARISHA MIFUMO YA UTEKELEZAJI WA SHERIA 2

| | | |
|---|---|---|
| 3.18 | LENGO MAHUSUSI 15: KUWEKA MAZINGIRA WEZESHAJI, FANISI NA YA KIMUONGOZO KWA JUMUIA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGO) KUFANYAKAZI NA SERIKALI | 2 |
| 4 | WADAU: UMUHIMU NA KAZI ZAO | 2 |
| 4.1 | SERIKALI | 2 |
| 4.1.1 | Serikali Kuu | 2 |
| 4.1.2 | Serikali za Mitaa | 2 |
| 4.2 | BARAZA LA WAWAKILISHI | 2 |
| 4.3 | MAHAKAMA | 2 |
| 4.4 | TAASISI ZA UANGALIZI | 2 |
| 4.4.1 | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 2 |
| 4.4.2 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma (PSC) | 2 |
| 4.4.3 | Mamlaka za Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi. | 2 |
| 4.4.4 | Vyombo vya habari | 2 |
| 4.4.5 | Jumuiya za Kiraia | 2 |
| 4.4.6 | Sekta Binafsi | 2 |
| 4.4.7 | Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) na Taasisi za kidini | 2 |
| 4.4.8 | Washirika wa Maendeleo. | 2 |
| 5 | MUUNDO WA UTEKELEZAJI WA SERA | 2 |
| 5.1 | UTEKELEZAJI WA SERA | 2 |
| 5.2 | MAREKEBISHO YA SERA | 2 |
| 5.3 | UFUATILIAJI NA TATHIMINI | 2 |

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **CAG** | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| **CHRAGG** | Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora |
| **CSOs** | Jumuiya za Kiraia |
| **ISO** | Shirika la Viwango la Kimataifa |
| **KKUB** | Kamati ya Kusimamia Utawala Bora |
| **MCAGGSP** | Mpango Mkakati wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora |
| **MDAs** | Wizara, Idara na Taasisi zake |
| **MKUZA** | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar |
| **NGO** | Jumuiya Zisizo za Kiserikali |
| **PSC** | Kamisheni ya Utumishi wa Umma |
| **TV** | Televisheni |
| **UNDP** | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| **WITS** | Wizara, Idara na Taasisi za Serikali |
| **WUUUB** | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| **ZBC** | Baraza la Biashara Zanzibar |
| **ZGGSP** | Mpango Mkakati wa Utawala Bora Zanzibar |

# DIBAJI

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na watu wake wanatambua na kuthamini umuhimu wa kuimarisha utawala bora na umoja wa kitaifa nchini, jambo lililodhihirishwa kutokana na juhudi mbalimbali ambazo serikali inazichukua katika eneo hili pana. Serikali imefanya mageuzi kadhaa ya kiutawala ambayo yameweka mazingira ya kuwezesha ukuaji wa uchumi pamoja na kutayarisha sera mbalimbali za kuondoa umaskini. Baadhi ya mageuzi makubwa yanayoendelea kufanywa hivi sasa ni pamoja na mageuzi ya Utumishi wa Umma, Serikali za Mitaa, Mazingira ya Biashara na Usimamizi wa Fedha za umma. Serikali pia imechukua hatua za kuimarisha ushirikishwaji wa Jumuiya za kiraia kama vile jumuiya zisizo za kiserikali, Jumuiya za kidini na jumuiya za wananchi pamoja na sekta binafsi katika mijadala na midahalo juu ya maendeleo ya taifa na kuchangia katika uundaji wa sera. Ushirika wa Serikali na sekta binafsi umeimarishwa kwa kuundwa Baraza la Biashara la Zanzibar.


Hata hivyo katika suala zima la uendeshaji bado kuna maeneo yanayolalamikiwa. Maeneo hayo ni pamoja na utendaji na miundo isiyotosheleza ndani ya Serikali mambo yanayopelekea kuweko na majukumu yasiyowazi na yasiyoendana katika sekta kadhaa, ambayo pia husababisha kuweko kwa taratibu za kufanya maamuzi zenye usumbufu, uwezo mdogo wa utendaji, mahusiano hafifu baina ya Serikali na wananchi na kushindwa kutekeleza kwa ufasaha dhana ya mgawanyo wa madaraka na majukumu miongoni mwa Baraza la Wawakilishi, Serikali na Mahakama.

Hivyo basi, ni muhimu kuwepo kwa sera ya taifa ya Utawala Bora ambayo itahakikisha kwamba mchakato wa uendeshaji hapa Zanzibar unaendeshwa kwa kufuata misingi ya katiba; mgawanyo wa madaraka na utawala wa sheria; na kuimarisha maadili ya utendaji na utamaduni.
Sera ni tamko linaloelezea namna mambo yanavyopaswa kushughulikiwa. Sera ya Utawala Bora imetayarishwa mahususi kuasisi, kukuza na kuimarisha misingi ya utawala bora kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya wananchi kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni nchini. Kwa maneno mengine sera hii inatarajiwa kuweka mazingira yanayowezesha

uimarishaji wa Utawala Bora. Inatarajiwa iwe ndiyo chombo cha kuimarisha na kuamsha hisia za kuheshimu misingi ya utawala bora hapa Zanzibar. Aidha sera inaweka wazi msimamo wa Serikali wa kuunga mkono masuala ya utawala bora. Kuweko kwa sera kutaongeza matumaini kwa wadau wakuu wa nje (wafadhili, washirika wa maendeleo, Jumuiya Zisizo za Kiserikali, n.k) na kusaidia uelewa wa watendaji wa kisiasa na kukidhi matarajio yao. Sera pia itaimarisha maendeleo na kukuza uelewa wa ndani, uwezo wa kiutawala na uongozi juu ya Utawala Bora.

Matumaini yangu ni kwamba sera hii itafahamika na kukubalika kwa vile ni matokeo ya vikao vingi, virefu na vyenye maana vya mijadala na mazingatio baina ya wadau kutoka sekta na makundi mbalimbali. Wakati wa utayarishaji wake sera hii iliwashirikisha wawakilishi kutoka serikalini na taasisi zisizo za kiserikali (za kitaifa na kimataifa), sekta ya sheria, makundi ya akina mama, wanasiasa, viongozi wa kijamii na wataalamu wa nyanja tofauti pamoja na wawakilishi wa Jumuiya za kimataifa ambao walitoa michango yao kuhusu fursa na changamoto katika eneo la Utawala Bora.

Katika mazingatio yao masuala kadhaa hasi na chanya yalijadiliwa kwa makini. Masuala kama vile Dira, Dhamira, Malengo na Muundo wa utekelezaji na Ufuatiliaji na Tathmini ya sera yalijadiliwa kwa makini na kutolewa maamuzi. Hivyo basi, kwa vile wadau wetu wamesaidia kutayarisha sera hii ni dhahiri watasaidia pia katika ushajiishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa kila siku na tathmini ili kufikia lengo lililokusudiwa.
Hivyo ni matumaini yangu ya dhati kwamba wadau wote wataifanya sera hii kuwa chombo muhimu cha kuimarisha Utawala Bora Zanzibar.



**Haji Omar Kheri**
**Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais)**
**Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Zanzibar**

# 1 UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ni kielelezo muhimu cha uimarishaji wa misingi ya utawala bora Zanzibar kwani ndiyo yaliyowakomboa Wazanzibari kutoka ukoloni wa kisultani na kuleta Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Mara baada ya Mapinduzi hayo Serikali ilichukua hatua kadhaa zilizolenga kuimarisha utawala bora nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuundwa kwa Wizara ya Kuweka Hali za Wananchi Sawa ambayo ilikuwa na jukumu la kukuza ustawi wa wananchi; na kuanzishwa kwa Ofisi Kuu ya Maendeleo (OKM) ili kusimamia masuala ya uongozi wa fedha. Mwaka 1979 liliundwa Baraza la Wawakilishi likiwa na uwakilishi wa wananchi. Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 iliundwa Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora na kupewa majukumu ya kusimamia masuala ya utawala bora. Wizara hiyo ilikuwa na jukumu la kuratibu kwa mapana zaidi masuala ya katiba, utawala bora, sheria pamoja na kusimamia taasisi za kidini. Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 na kuzinduliwa kwa Serikali ya awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa, iliundwa Wizara ya Nchi (Ofisi ya Rais) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kuundwa kwa wizara hii kunaonesha ni kwa kiasi gani Rais amelipa kipaumbele suala hili.

Masuala ya Utawala Bora nchini yameelezwa katika nyaraka tofauti za Serikali kama vile Dira ya mwaka 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) na Mpango Mkakati wa Utawala Bora Zanzibar wa mwaka 2003 pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora wa mwaka 2007-2012. MKUZA umetambua umuhimu wa kuimarisha Utawala Bora na umoja wa kitaifa na kuweka mazingira bora na ya kudumu kwa maendeleo endelevu. Kwa mtazamo huu, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imefanya mageuzi kadhaa ya kiutawala yanayolenga kuweka mazingira yanayohitajika katika kuimarisha ukuaji wa uchumi na uundwaji wa sera za kupunguza umaskini na kuimarisha Utawala Bora. Baadhi ya mageuzi yanayoendelea kufanywa hivi sasa ni pamoja na mageuzi ya utumishi wa umma, serikali za mitaa, mazingira ya biashara na usimamizi wa fedha za umma.

## 1.2 Haja ya kuwa na Sera ya Utawala Bora

Ingawa kumekuwa na programu nyingi za mageuzi bado kuna changamoto. Kwa mfano upatikanaji wa haki bado ni wa kiwango cha chini kwa sababu ya uhaba wa mahakimu na mifumo isiyotosheleza ya misaada ya kisheria. Utoaji wa huduma ni wa kiwango cha chini katika takriban sekta zote na pia kuna migongano kuhusu miundo ya uendeshaji; mageuzi hayamilikiwi na Serikali kwa ukamilifu wake; uelewa mdogo wa wananchi katika kuifanya Serikali iwajibike na kiwango kidogo cha uwazi katika mikataba yenye maslahi kwa taifa.

Misingi ya Utawala Bora haikujumuishwa katika sera nyingi za taifa na mikakati mingi ya maendeleo; na zaidi katika taratibu za utendaji wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Mawazo ya baadhi ya wadau kwamba uimarishaji wa utawala bora ni jukumu la wizara moja pekee yameongeza tatizo na hata kulifanya suala la kuratibu juhudi za kuimarisha utawala bora kuwa gumu zaidi. Wakati kuna wizara kadhaaa zinazoshughulikia kwa karibu zaidi masuala ya utawala bora kama vile Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majukumu yao katika kuimarisha viwango vya uendeshaji (governance standards) hayakuwekwa wazi. Hili limepelekea kutokuweko mtiririko mzuri na mlingano wa malengo katika sekta mbalimbali. Hivi sasa pia kuna vyombo vingi vya kisera lakini majukumu yao hasa katika kushughulikia masuala ya utawala bora nchini hayajulikani vyema hivyo maeneo halisi ambayo yanahitaji kutungiwa sheria na hatua nyengine hayajulikani sawa sawa.

Kuna ithibati chache kuonesha kiwango halisi cha utawala bora Zanzibar na hii inapelekea ulazima wa kuweka vigezo na namna ya kupima na kuimarisha kiwango cha utawala bora. Pamoja na kwamba Serikali ilitayarisha Mpango Mkakati wa Utawala Bora Zanzibar na Mpango Mkakati wa Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora, bado haijatayarisha sera ya utawala bora itakayosaidia juhudi za Serikali katika kuimarisha utawala bora. Hivyo basi sera hii itaweka mazingira mazuri ya kuimarisha utawala bora Zanzibar.

## 2.0 MAANA NA MISINGI YA UTAWALA BORA

### 2.1 Maana ya Utawala Bora

Utawala ni namna ambavyo Serikali inafanya kazi zake katika maeneo yake na namna ambavyo inaweka mahusiano na wananchi, Jumuiya za kiraia pamoja na taasisi nyengine. Utawala Bora ni utumiaji wa madaraka kwa ufanisi, uaminifu, usawa, uwazi na uwajibikaji katika ngazi tofauti za Serikali

### 2.2 Misingi ya Utawala Bora

**Utawala Bora unatafsiriwa kwa misingi ifuatayo:**

#### 2.2.1 Uwajibikaji na Uwazi

Uwajibikaji maana yake ni madaraka yanayotumika ndani ya jamii na taifa kwa jumla na pia ni wajibu kwa wenye madaraka kutoa maelezo ya maamuzi yao. Uwajibikaji unahitaji kuhakikisha kwamba madaraka ya umma, yawe ya kibusara au ya aina nyengine yanatumika siyo tu kwa mujibu wa sheria bali pia yanatumika kwa mujibu wa taratibu bora za kiutawala. Aidha kwa taratibu za uwajibikaji kutekeleza au kuacha kutekeleza jambo lolote ni lazima kutolewe maelezo na kujengewa hoja. Watu, mamlaka na taasisi zote zitabeba dhamana kwa matokeo ya maamuzi au vitendo vyao.

Uwazi ni utoaji wa taarifa sahihi na za kuaminika kwa watu wote. Inavyohitakiwa ni kwamba umma kwa jumla au angalau wale wanaoguswa moja kwa moja na maamuzi yanayofanywa na Serikali, watumishi wa umma pamoja na watoa huduma binafsi wanapata taarifa kutoka kwa Serikali au watumishi hao.

#### 2.2.2 Utawala wa Sheria na Haki za Binadamu

Utawala wa sheria umegawika sehemu tatu. Sehemu hizi ni sheria kushika hatamu (hakuna mtu aliyeko juu ya sheria), mgawanyo wa madaraka (uhuru wa mihimili mitatu ya dola – Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama) na kwamba hakuna mtu atakayepewa adhabu isipokuwa kwa kuvunja sheria na hakuna mtu atakayetiwa hatiani kwa kuvunja sheria isipokuwa kwa taratibu zilizowekwa na sheria yenyewe. Mgawanyo wa madaraka unamaanisha kwamba Serikali, Mahakama na Baraza la Wawakilishi kila moja linafanyakazi kwa uhuru bila kuingiliwa na taasisi nyengine, wakati uhuru wa Mahakama unamaanisha kwamba mahakama ziko huru kuendesha kesi bila kuingiliwa na taasisi nyengine yoyote.

Hivyo basi, mtu mmoja mmoja pamoja na Serikali wataheshimu, watatii, na kuongozwa na sheria na siyo mtu au kikundi cha watu kuchukua sheria mkononi. Ili nchi iwe inaheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu ni lazima sheria ziwe ni zile ambazo wananchi wanazitarajia, zijulikane vyema na lazima ziwe zenye kuwahusu wote na zisizobagua. Suala la utawala wa sheria limeelezwa vyema katika Katiba ya Zanzibar ya 1984. Aidha suala la utawala wa sheria linatokana na maazimio ya kimataifa kuhusu haki za binadamu ambayo nchi yetu imeridhia na yamefafanuliwa vizuri katika sheria za Zanzibar kwa kuzingatia viwango hivyo vya kimataifa.

### 2.2.3 Kuzuia rushwa

Rushwa maana yake ni matumizi mabaya ya Ofisi ya umma kwa maslahi binafsi. Ni muhimu basi kuelewa kwamba rushwa ni tofauti na wizi na ukwepaji wa majukumu. Kuna uwezekano wa kuzuka vitendo vya rushwa pale ambapo ama kuna mifumo dhaifu ya kiutawala, uwazi na uwajibikaji au mifumo hiyo inatumiwa vibaya, na inapotokea hali hiyo inakuwa ni dalili ya uendeshaji usiofaa.

### 2.2.4 Ufanisi na tija

Ufanisi maana yake ni utekelezaji majukumu kwa kufikia malengo yaliyowekwa. Tija ni kufanya uzalishaji ulio bora au kutoa huduma bora kwa gharama nafuu kadri inavyowezekana. Hii inamaanisha kwamba fedha na rasilamli watu zinatumika kwa namna iliyo bora kabisa bila ya ubadhirifu, wizi au kucheleweshwa.

### 2.2.5 Ushirikishwaji

Ushirikishwaji maana yake ni kubuni na kutekeleza kazi kwa pamoja na wadau husika. Ushirikishwaji wa wananchi, wadau na taasisi tofauti katika kufanya maamuzi na katika kutekeleza maamuzi hayo unatokana na kutambua kwamba mara nyingi sauti ya umma inawafanya watu kuona kwamba wao ni sehemu ya maamuzi yanayofanyika, unaimarisha uhalali wa maamuzi hayo na unakuza uwezo wa wahusika.

### 2.2.6 Kuzingatia matakwa ya wananchi

Kuzingatia matakwa ya wananchi maana yake ni uwezo na utayari wa kushughulikia matakwa, maslahi na vipaumbele vya wananchi. Hii inamaanisha kuwa tayari kukubali mabadiliko ya kijamii, kutambua maslahi ya jumla ya wananchi na kuwa tayari kuangalia upya majukumu ya serikali.

# 3 DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA

## 3.1 Dira

Zanzibar inataka kujenga taifa na jamii ambayo ndani yake misingi ya Utawala Bora inaimarishwa na kuheshimiwa.

## 3.2 Dhamira

Kujenga mazingira wezeshaji na endelevu kwa ajili ya uimarishaji wa Utawala Bora kwa kuheshimu Haki za Binadamu na utawala wa sheria, kuzuia rushwa na kuhakikisha kwamba misingi ya uwajibikaji, uwazi, ufanisi na tija, ushirikishwaji na kuzingatia matakwa ya wananchi inaheshimiwa.

## 3.3 Lengo Kuu

Lengo la kuu la sera hii ni kuweka, kuimarisha na kukuza misingi ya Utawala Bora kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni nchini.

### 3.3.1 Malengo mahususi

Malengo mahususi ya sera ya Utawala Bora Zanzibar ni:

1. Kuziwezesha wizara, idara na taasisi za Serikali na Jumuiya za kiraia kufuata misingi ya utawala Bora
2. Kuweka mifumo ya kupima viwango vya kuheshimu na kutekeleza misingi ya Utawala Bora katika ngazi zote
3. Kufanya mapitio ya sheria na miundo ya taasisi ambayo inaelezea majukumu ya wizara, idara na taasisi za Serikali
4. Kuweka taratibu za kuimarisha uratibu na utekelezaji fanisi wa programu za Utawala Bora
5. Kuhakikisha kwamba haki ya kupata habari inaheshimiwa vilivyo.
6. Kuhakikisha kwamba tathmini ya uhakiki wa Utawala Bora inafanyika hapa Zanzibar.
7. Kuweka mifumo madhubuti ya kuzuia rushwa
8. Kujenga sekta ya umma iliyofanisi, yenye tija na sikivu
9. Kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa
10. Kuimarisha taasisi za uangalizi
11. Kuimarisha uwajibikaji wa viongozi waliochaguliwa kwa wananchi
12. Kuhakikisha uheshimu wa majukumu ya kijamii

13. Kuweka mazingira wezeshaji, yenye ufanisi na miongozo kwa ajili ya Usimamizi bora wa mashirika
14. Kuimarisha mifumo ya utekelezaji wa sheria
15. Kuweka mazingira wezeshaji, yenye ufanisi na miongozo kwa asasi za kiraia kufanyakazi na Serikali

### 3.4 Lengo mahususi 1: Kuziwezesha wizara, idara na taasisi za Serikali na jumuiya za kiraia kufuata misingi ya utawala Bora

Ufahamu wa wizara, idara na taasisi za Serikali na jumuiya za kiraia juu ya misingi ya Utawala Bora na matumizi yake ni mdogo.

**Tamko la Sera**

Misingi ya Utawala Bora itazielekeza wizara, idara na taasisi za Serikali katika kutunga na kutekeleza sera, sheria na kanuni kwa shughuli za ndani ya Serikali pamoja na maingiliano yao na wananchi na jumuiya nyengine Zanzibar.

**Mkakati wa Sera**

i. Katibu Mkuu Kiongozi ataweka taratibu zitakazohakikisha kwamba kila wizara inateua mwakilishi mwenye cheo cha Mkurugenzi kushughulikia masuala ya Utawala Bora. Katibu Mkuu Kiongozi atahakikisha kwamba taratibu zilizowekwa zinafuatwa.

ii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itaanzisha kikundi-kazi cha Utawala Bora (KKUB). Wajumbe wa kikundi-kazi hicho watakuwa ni wawakilishi wote ambao wameteuliwa kwa mujibu kifungu (i) hapo juu. Mwenyekiti wa kikundi-kazi hicho atatoka wizara inayoshughulikia Utawala Bora ambayo ndiyo itakayoongoza shughuli zote za kikundi-kazi hicho.

iii. Wizara, idara na taasisi za Serikali na jumuiya za kiraia zitajumuisha masuala ya Utawala Bora katika kazi zao.

iv. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora, kwa mashauriano na kikundi-kazi cha utawala bora, itatayarisha mipango ya Mafunzo na uhamasishaji kwa wafanyakazi wa wizara, idara na taasisi za Serikali na Jumuiya za kiraia ili kuimarisha ufahamu wao juu ya dhana ya Utawala Bora.

### 3.5 Lengo mahususi 2: Kuweka mifumo ya kupima viwango vya kuheshimu au kutekeleza misingi ya Utawala Bora katika ngazi zote.

Hakuna viashiria vya Utawala Bora katika wizara, idara na taasisi za Serikali na kwa hivyo hali halisi pamoja na maendeleo ya Utawala Bora hayawezi kutolewa ripoti kwa ufanisi.

**Tamko la Sera**

Misingi ya Utawala Bora itatumiwa na wizara, idara na taasisi zote za Serikali na jumuiya za kiraia kutayarisha na kutoa ripoti kwa kutumia viashiria vya Utawala Bora.

**Mkakati wa Sera**

i. Katibu Mkuu Kiongozi ataitaka kila wizara kutayarisha viashiria vya Utawala Bora ambavyo vitatumika kupima hali halisi ya Utawala Bora ya kila wizara katika maeneo yake mahususi.

ii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itatayarisha viashiria vya kitaifa vya Utawala Bora.

iii. Mwakilishi wa kila wizara katika kikundi-kazi cha Utawala Bora ndiye atakayehusika kutoa ripoti za robo mwaka za hali halisi ya Utawala Bora za wizara yake kwa wizara inayoshughulikia Utawala Bora. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itatoa taarifa ya hali halisi ya Utawala Bora kila mwaka kupitia ripoti ya mwaka ya Utawala Bora ya Zanzibar.

iv. Serikali itazishajiisha na kuziwezesha taasisi Zisizo za Kiserikali kutayarisha viashiria vya utawala bora katika maeneo yao na kuwasilisha ripoti ya robo mwaka na ya mwaka kwa wizara inayoshughulikia utawala bora

### 3.6 Lengo mahususi 3: Kufanya mapitio ya sheria na miundo ya taasisi inayoelezea majukumu ya wizara, idara na taasisi za Serikali.

Kuna wizara kadhaa zenye majukumu yanayohusu Utawala Bora lakini majukumu yao hayajafafanuliwa vyema. Kuna vyombo vyengine vingi vya kisera lakini majukumu yao halisi katika kushughulikia Utawala Bora Zanzibar hayajulikani kwa ukamilifu. Hivyo basi mawanda halisi

ya hatua za kisheria na hatua nyengine ambazo ni za lazima kuchukuliwa hazijulikani kwa ukamilifu.

Vyombo vya kisera vilivyopo hivi sasa ni pamoja na:

- Katiba ya Zanzibar ya 1984
- Muongozo wa Haki za Binadamu (2008)
- Sheria ya Adhabu (Marekebisho) Namba 6 ya 2004
- Sheria ya Fedha Namba 12 ya 2005
- Sheria ya Jumuiya Namba 6 ya 1995
- Sheria ya Kampuni
- Sheria ya Manunuzi Namba 9 ya 2005
- Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2011

**Tamko la Sera**

Serikali itafafanua mamlaka na wajibu wa taasisi za Serikali na kufanya mapitio ya miundo iliyopo ya kisheria na ya kitaasisi ili kugundua hatua mpya zinazopaswa kuchukuliwa kuwawezesha wahusika kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika kuimarisha Utawala Bora Zanzibar.

**Mkakati wa Sera**

i. KKUB chini ya uongozi wa wizara inayoshughulikia Utawala Bora kitafanya mapitio ya vyombo vya sera vilivyopo, kutoa taarifa za mapitio hayo na kupendekeza hatua za kuchukuliwa.

ii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itafanya mapitio na kufafanua majukumu na kazi za wizara, Idara na taasisi za Serikali kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma.

iii. Serikali itafanya mapitio na kufafanua majukumu ya Serikali kuu na Serikali za mitaa pamoja na kuweka miundo ya uwajibikaji ndani ya Serikali kuu na Serikali za mitaa na baina ya Serikali kuu na Serikali za mitaa.

iv. Serikali itafanya mapitio ya mifumo ya sasa ya uratibu na ya hali halisi ya utekelezaji wa dhana ya mgawanyo wa mdaraka kati ya Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama kwa lengo la kuimarisha Utawala Bora Zanzibar.

### 3.7 Lengo mahususi 4: Kuweka taratibu za kuimarisha uratibu na utekelezaji fanisi wa programu za Utawala Bora

Uratibu wa taasisi zenye jukumu la kuimarisha Utawala Bora hivi sasa ni mdogo. Mawazo ya baadhi ya wadau kwamba jukumu la kuimarisha Utawala linaihusu wizara moja pekee linapelekea suala la uratibu wa Utawala Bora kuwa gumu zaidi. Mawasiliano na Uratibu wa masuala ya Utawala Bora na utekelezaji wa sera hii ni lazima uwekewe muundo ulio wazi.

**Tamko la Sera**

Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itahakikisha kunakuweko mawasiliano na Uratibu mzuri wa masuala ya Utawala Bora serikalini kote.

**Mkakati wa Sera**

i. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itafanya mikutano ya kikundi-kazi cha Utawala Bora kwa uchache kila baada ya miezi mitatu kwa utaratibu utakaopangwa kabla kwenye bajeti ya mwaka.

ii. Kwa ajili ya Uratibu mzuri wa masuala ya Utawala Bora wajumbe wa kikundi-kazi cha Utawala Bora watawasilisha taarifa na/au rikodi za Utawala Bora kwa wizara inayoshughulikia Utawala Bora

iii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora inaweza kuzitumia taarifa zilizokusanywa kutoka wizara nyengine kutayarisha ripoti ya mwaka ya Utawala Bora ya Zanzibar.

iv. KKUB kitajenga mahusiano mazuri kikazi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG).

v. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itatayarisha Mkakati wa mawasiliano kurahisisha uratibu wa Utawala Bora.

### 3.8 Lengo mahususi 5: Kuhakikisha kwamba haki ya kupata habari inatekelezwa kikamilifu

Kumekuwa na malalamiko kutoka vyombo vya habari na taasisi nyengine kwamba dhana ya haki ya kupata habari haitekelezwi kikamilifu. Uimarishaji wa Utawala Bora Zanzibar, kama ilivyo kwa nchi nyengine yoyote duniani, unategemea sana uhuru wa kupata habari kwa taasisi za uangalizi na kwa wananchi wa Zanzibar.

**Tamko la Sera**

Serikali itahakikisha kwamba taasisi za uangalizi na wananchi wa Zanzibar wanapata habari kuhusu maamuzi na utendaji wa viongozi walioteuliwa na watendaji wa wizara, idara na taasisi za Serikali.

**Mkakati wa Sera**

i. Serikali itatayarisha sheria ya Uhuru wa Habari

ii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora kwa kushirikiana na kikundi-kazi cha Utawala Bora itatayarisha programu za uelimishaji kwa wizara, Idara na taasisi za Serikali kuhusu majukumu na wajibu wa uhuru wa Habari kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambayo yatakuwa sehemu ya sheria ya Uhuru wa Habari

iii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora kwa kushirikiana na kikundi-kazi cha Utawala Bora itafanya kampeni ya kuelimisha umma ili kuhakikisha kwamba taasisi zote za uangalizi na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wanazielelwa haki zao za kupata habari kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984 na ambazo zitakuwa sehemu ya sheria ya Uhuru wa Habari.

iv. Serikali itahakikisha kwamba Utumishi wa Umma unajenga utamaduni wa kuwahudumia wananchi, taasisi za uangalizi na wahusika wengine kwa kuwapa habari zilizo sahihi na kwa wakati.

### 3.9 Lengo mahususi 6: Kuhakikisha kwamba tathmini ya kina ya Utawala Bora inafanyika hapa Zanzibar.

Ili kufanya maamuzi yanayofahamika juu ya namna ya kugawanya rasilimali kwa kuimarisha utawala Bora hapa Zanzibar, ukweli kuhusu mitazamo, uelewa pamoja na uzoefu kuhusu Utawala Bora lazima vijuilikane.Kutokana na maumbile ya kazi hiyo, hakuna budi tafiti hizi ziendeshwe na taasisi huru.

**Tamko la Sera**

Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itahakikisha kwamba tathmini ya kina juu ya utawala bora inafanywa kama kawaida kwa kutumia mpango mkakati uliopo.

**Mkakati wa Sera:**

i. Wizara inayoshughulikia utawala Bora itahakikisha kwamba tathimini ya mwelekeo na matumizi ya utawala bora katika utumishi wa umma, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na miongoni mwa watu mbali mbali inafanyika kila mwaka.

ii. Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na Kikundi Kazi cha Utawala Bora (KKUB) itatumia matokeo ya tafiti hizo katika utekelezaji na tathmini ya sera ya Utawala Bora.

iii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora kwa kusaidiana na (KKUB) zitatoa matokeo yote ya utafiti kwa Umma pamoja na ripoti ya Mwaka ya Utawala Bora ya Zanzibar.

iv. Wizara inayoshughulikia Utawala bora kwa kusaidiana na (KKUB) itatayarisha Mpango Mkakati wa Utawala Bora ambao utaweka vigezo ambavyo vinaweza kutathminiwa.

## 3.10 Lengo mahususi 7: Kuweka mifumo madhubuti ya kuzuia rushwa

Moja kati ya mambo ambayo yanahatarisha Utawala Bora ni rushwa. Rushwa inarejesha nyuma ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa jumla. Jambo hili hutokea katika nchi nyingi duniani na hasa kwenye taasisi za Umma, sekta binafsi pamoja na jumuiya zisizo za kiserikali.

**Tamko la Sera**

Serikali itapambana na mizizi ya rushwa na kushajiisha ushiriki wa Umma katika vita dhidi ya rushwa kwenye taasisi za umma na jamii kwa ujumla.

**Mkakati wa Sera:**

i. Serikali itatayarisha mswada wa kupambana na rushwa.

ii. Mswaada wa Sheria ya kuzuia rushwa utapendekeza uanzishwaji wa mamlaka ya kupambana na rushwa ambayo itapambana dhidi ya uongozi mbaya na vitendo vya rushwa. Sheria pia itapendekeza kuanzishwa utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na namna ya kuyatolea taarifa.

iii. Wizara inayoshughulikia utawala bora, kwa kusaidiana na ( KKUB) itafanya kampeni kwa ajili ya kutoa mwamko kwa jamii juu ya ubaya wa rushwa na faida ya kuwa na jamii isiyo na rushwa, na vile vile kutoa taaluma juu ya Mswada wa Kuzuia rushwa.

iv. Wizara, idara na taasisi za Serikali (WITS) zitatekeleza dhana ya uwazi na uwajibikaji katika mipango na utumiaji wao wa rasilimali. (WITS) zitaheshimu taratibu za manunuzi na matumizi. Kila (WITS) itatoa taarifa ya kila mwaka juu hatua ilizochukua katika kutekeleza kifungu hiki. Wajumbe (Focal Persons) katika (KKUB) watakuwa ndio wenye dhamana ya kuandaa ripoti hii na kuiwasilisha kwa wizara inayoshughulikia Utawala Bora. Ripoti hiyo itakuwa sehemu ya ripoti ya mwaka ya Utawala Bora ya Zanzibar ambayo itatolewa kwa umma.

v. Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na (KKUB), itahakikisha kwamba uhakiki wa kiwango cha rushwa unajumuishwa katika tafiti za kila mwaka na matokeo yake yanaingizwa kwenye ripoti ya mwaka ya utawala bora Zanzibar.

### 3.11 Lengo mahususi 8: Kujenga taasisi zenye ufanisi, tija na sikivu Utumishi wa Umma wa Zanzibar haujafikia kiwango cha ufanisi wala tija na kwa hivyo haukidhi matarajio ya wananchi kwa changamoto za maendeleo.

Utafiti juu ya Taasisi za umma uliofanywa hapa Zanzibar mwaka 2009 umegundua kwamba Wizara, Idara na Taasisi nyingi za Serikali haziwezi kutekeleza majukumu na kazi zao kwa tija na ufanisi.

**Tamko la Sera**

Serikali itahakikisha kwamba sekta ya umma inatoa huduma kwa ufanisi na tija kwa namna ambayo itakuwa sikivu kwa matakwa ya Umma.

**Mkakati wa Sera:**

i. Serikali itahakikisha kwamba utumishi wa umma unatekeleza misingi ya utawala bora katika kutoa huduma zake. Lengo la msingi ni kuona kwamba Sera ya utumishi wa umma Zanzibar ya mwaka (2010) inatekelezwa ipasavyo.

ii. Kama ilivyo katika sheria ya utumishi wa umma, Kamisheni ya Utumishi wa Umma itaitaka kila Wizara, Idara na taasisi yenye majukumu ya moja kwa moja ya kutoa huduma kuweka malengo sahihi, na yanayopimika katika utoaji huduma. Malengo kama hayo yatatayarishwa kwa ajili ya mashirika ya umma na makandarasi wa sekta binafsi wanaotoa huduma kwa umma. Kila (WITS) itatayarisha ripoti yake ya mwaka juu ya utekelezaji wa malengo hayo. Ripoti hizo zitatolewa kwa Umma.

iii. Wizara inayoshughulikia utawala Bora itaiomba Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuchambua masharti ambayo yanaathiri utumishi wa umma Zanzibar. Kamisheni ya utumishi wa Umma

itawasilisha ripoti hiyo kwa Wizara inayoshughulikia utawala bora.

iv. Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na (KKUB) itaziomba wizara, idara na taasisi husika kuanzisha na/au kuimarisha mifumo ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika sekta ya umma.Wizara, idara na taasisi hizi za Serikali zitatoa ripoti za robo mwaka juu ya viashiria vya utawala bora kwa wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kupitia mjumbe (focal person) katika (KKUB).

v. Serikali itajitahidi kukuza ubia kati ya sekta ya umma na Binafsi kwa utoaji huduma wenye ufanisi na tijana ambao ni sikivu kwa matakwa ya umma.

**3.12 Lengo mahususi 9: Kuimarisha Serikali za Mitaa.**

Serikali za Mitaa zinajukumu la kuhakikisha kwamba uwazi uwajibikaji na ushirikishwaji wa watu unaimarishwa. Mpaka hivi sasa serikali za mitaa Zanzibar hazitekelezi kazi zake kwa ufanisi kutokana na kutokuwepo kwa uwiano na miundo inayotatiza ya uwajibikaji, kiwango kidogo cha uwazi na ukosefu wa fedha na uwezo mdogo wa rasilimali watu.

**Tamko la Sera**

Serikali itahakikisha kwamba mamlaka na uwezo wa serikali za mitaa unaimarishwa, ili kukuza ushiriki wa wananchi katika utoaji wa maamuzi.

**Mkakati wa Sera:**

i. Serikali itatayarisha sheria ya kukasimu madaraka ya utoaji wa maamuzi, utoaji wa huduma na mgawanyo wa fedha, kwa madiwani kwa ajili ya kuwawezesha kupanga mipango ya maendeleo.

ii. Serikali itahakikisha inaharakisha mageuzi ya serikali za mitaa ili kuwa na ushiriki wa wananchi wenye ufanisi na manufaa katika maamuzi yanayogusa maisha yao.

iii. Serikali kuu na serikali za mitaa zitakuza upashanaji habari baina yao wenyewe pamoja na kukuza upashanaji habari baina yao na taasisi za uangalizi na jumuia zisizo za kiserikali.

iv. Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na (KKUB) itahakikisha kwamba mifumo ya mafunzo na maendeleo ya rasilimali watu katika serikali za mitaa inaazishwa.

### 3.13 Lengo mahususi 10: Kuimarisha Taasisi za Uangalizi.

Kuna juhudi za makusudi za kuzikuza taasisi za uangalizi kwa vile zina nafasi kubwa katika utawala bora.Taasisi za uangalizi bado zinaupungufu wa rasilimali na zina uwezo mdogo wa kutekeleza majukumu yao.

**Tamko la Sera**

Uwezo wa taasisi za uangalizi kifedha utaongezwa ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Mkakati wa Sera:**

i. Mchakato wa bajeti ya mwaka utaweka mkazo maalum kwa mahitaji ya kamati ya Hesabu za Serikali ya Baraza la Wawakilishi, na vile vile mahitaji ya Baraza la Wawakilishi kufanya shughuli za uangalizi kwa ufanisi.

ii. Mchakato wa bajeti ya mwaka utaweka pia mkazo maalum kwa mahitaji ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa kwa shughuli zao za uangalizi.

iii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itakuwa na jukumu mahususi la kuhakikisha kwamba taasisi za uangalizi zinajengewa uwezo, vikiwemo vyombo vya habari, ili kutekeleza majukumu yao ya kutoa habari na kuweka kumbukumbu kuhusu utawala bora Zanzibar.

iv. Wizara inayoshughulikia Utawala bora itakuwa na mamlaka ya kuandaa na kushajiisha mambo ya utawala bora kwa jumuiya za

kiraia na vyombo vya habari kwa ajili ya kuziimarishia uwezo wao na kufanya kazi kama taasisi za uangalizi.

### 3.14 Lengo Mahususi 11: Kuimarisha Uwajibikaji wa viongozi waliochaguliwa kwa wananchi.

Wananchi pamoja na baadhi ya viongozi waliochaguliwa wana uelewa mdogo wa dhana ya uwajibikaji, uwazi, na haki ya kupata habari. Huenda hali hiyo inatokana na uzoefu mdogo wa viongozi hao juu ya dhana ya demokrasia. Uelewa lazima uimarishwe kwa kutumia mitazamo mbali mbali ambayo itahakikisha kwamba dhana ya utawala bora inafahamika na kila mtu katika jamii.

**Tamko la Sera**

Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itakuza uhusiano wa kiuwajibikaji baina ya viongozi wa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar. Lengo ni kwamba viongozi hao wawajibike kikamilifu kwa matendo na maamuzi yao; wawe wasikivu kwa matakwa ya wananchi; na matendo pamoja na maamuzi yao yawe ya uwazi.

**Mkakati wa Sera:**

i. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora kwa kusaidiana na (KKUB) itaandaa kampeni za kiuwajibikaji ambazo zitafanyika katika ngazi zote za jamii kwa kutumia redio, televisheni, magazeti, vipeperushi, senema, na majukwaa ya sanaa. Lengo kuu la kampeni hizo litakuwa ni kuelimisha umma juu ya haki na fursa ya kupata habari na msingi wa uwajibikaji.

ii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora inaweza kutumia matokeo ya utafiti (sehemu 5.1) kwa Kukuza uelewa wa jamii.

iii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itawashirkisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa vipindi (hasa wale wapya) katika semina za kukuza uelewa juu ya misingi ya utawala bora kwa watunga sheria.

### 3.15 Lengo mahususi 12: Kuhakikisha uheshimu wa majukumu ya kijamii.

Katika miaka ya karibuni taratibu na mifumo ya kimataifa juu ya majukumu ya kijamii ni mambo ambayo yameendelezwa. Mambo hayo ni pamoja na majukumu ya kibiashara, utawala wa makampuni na maadili kwa taasisi za washirika wa maendeleo. Katika kuimarisha Utawala Bora Zanzibar hakuna taratibu ambazo zinaongoza uheshimu wa majukumu ya kijamii.

**Tamko la Sera**

Serikali itahakikisha uheshimu wa majukumu ya kijamii Zanzibar kwa Jumuiya za kibiashara, jumuiya zisizo za kiserikali, taasisi za kidini, washirika wa maendeleo na taasisi nyingine.

**Mkakati wa Sera:**

i. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora kwa kusaidiana na (KKUB) itawaalika wadau husika katika kuanzisha na kuandaa taratibu za pamoja juu ya majukumu ya kijamii hapa Zanziabar, hasa kwa kuangalia muongozo wa viwango vya kimataifa juu ya majukumu ya kijamii.

ii. Wizara inayoshughulikia Utawala Bora itaunda kikundi kazi kitakachohusisha wawakilishi wa Serikali na wa wafanya biashara kuangalia uwezekano wa kuandaa ripoti ya mwaka ya majukumu ya kijamii kwa makampuni, kwa kuangalia hasa taratibu za ulimwengu za kutayarisha ripoti.

### 3.16 Lengo mahususi 13: Kuweka mazingira wezeshaji, fanisi na ya kimuongozo kuhusu utawala bora kibiashara

Kuna mifumo isiyotosheleza ya kuhakikisha kwamba sekta binafsi inaheshimu majukumu yake ya kisheria kuhusu haki za wadau

**Tamko la Sera**

Serikali itaweka mifumo thabiti kuhakikisha kwamba taasisi za kibiashara zinashiriki kikamilifu katika harakati za maendeleo na wakati huo huo zinaheshimu majukumu yao ya kisheria kuhusu haki za wadau

**Mkakati wa Sera**

i. Serikali itatayarisha muundo madhubuti wa utawala wa

kibiashara ambao utahakikisha kuweko kwa haki za wadau, majukumu muhimu ya umilikaji na kuhakikisha kwamba wadau wote wanatendewa sawa

ii. Serikali itaweka majukumu ya utawala bora kibiashara kwa uwazi, misingi ya maadili, miiko na utendaji inayowezesha kuweka uwiano baina ya malengo ya kiuchumi na ya kijamii.

iii. Serikali itaweka mifumo itakayohakikisha uwazi na uwajibikaji

## 3.17 Lengo mahususi 14: Kuimaarisha mifumo ya utekelezaji wa sheria

Hivi sasa kuna sheria nyingi hapa Zanzibar lakini mifumo ya utekelezaji wa sheria hizo ama haitoshelezi au haipo kabisa

**Tamko la Sera**

Serikali itaweka mifumo madhubuti ya utekelezaji wa sheria

**Mikakati ya Sera**

i. Kuinua uelewa wa Wananchi juu ya sheria zilizopo

ii. Kuanzisha na kuimarisha mahakama maalum kushughulikia sheria maalum

iii. Kuharakisha mwenendo wa kesi

**3.18 Lengo mahususi 15: Kuweka mazingira wezeshaji, fanisi na ya kimuongozo kwa Jumuia Zisizo za Kiserikali (NGO) kufanyakazi na Serikali**

Kuna Jumuiya nyingi Zisizo za kiserikiali ambazo zimesajiliwa hapa Zanzibar ambazo zina majukumu tofauti na ambazo zinakuwa ni kiungo baina ya Serikali na jamii kwa ujumla. Hata hivyo mahusiano ya kuitendaji baina ya Serikali na NGO hayako wazi.

**Tamko la Sera**

Serikali itahakikisha kwamba mifumo thabiti na ya kimuongozo kwa ajili ya NGO kufanyakazi na Serikali inakuwepo

**Mkakati wa Sera**

i. Serikali itahakikisha kwamba Sera ya NGO inatekelezwa kikamilifu

# 4 WADAU: UMUHIMU NA KAZI ZAO

Utekelezaji bora wa sera hii unategemea sana makubaliano ya pamoja juu ya majukumu na kazi za kila taasisi.Wadau wa Utawala Bora Zanzibar ni pamoja na Serikali, Baraza la Wawakilishi, Mahakama, taasisisi za uangalizi, na Jumuiya za kiraia. Majukumu na kazi za kila mdau yanaorodheshwa hapa chini:

## 4.1 Serikali

### 4.1.1 Serikali Kuu

Wizara, idara na taasisi za Serikali wanawajibu wa kutimiza mahitaji ya msingi, matakwa na matarajio ya wananchi, na kuhakikisha kwamba shughuli zao zote zinaongozwa na misingi ya utawala bora kama ilivyoelezwa katika sera hii.

Wizara inayoshughulikia utawala bora inajukumu la kuratibu utawala bora na utekelezaji wa sera hii. Majukumu ya wizara inayoshughulikia utawala bora yameonyeshwa katika sera hii hapo juu. Kikundi kazi cha Utawala Bora kinajukumu la kuisaidia wizara inayoshughulikia utawala bora katika kutekeleza majukumu yake ya uratibu na utekelezaji wa ufanisi wa sera hii.

### 4.1.2 Serikali za Mitaa

Serikali za mitaa zinajukumu la kuhakikisha kwamba uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi unakuzwa katika uongozi wa mabaraza na kuimarisha haiba ya wananchi kupitia viongozi wao wa kuchaguliwa na jumuiya za kiraia.

## 4.2 Baraza la Wawakilishi

Baraza la wawakilishi ndilo linalotunga sheria na kupitisha bajeti ya taifa kwa maana hiyo hii ni taasisi muhimu katika kuhakisha kwamba utawala bora unaimarika hapa Zanzibar.

Baraza la wawakilishi linatekeleza kazi muhimu ya uangalizi kupitia kamati ya hesabu za Serikali ambayo inazipitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
Ni jukumu la kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kutekeleza jukumu la uangalizi kwa kuhakikisha kwamba serikali inatekeleza ahadi zake kwa wananchi wa Zanzibar, kutekeleza sera zake na kufanyakazi kwa mujibu wa sheria.

Mjumbe mmoja mmoja wa Baraza la Wawakilishi wanalojukumu la uangalizi katika majimbo yao kwa kuhakikisha kwamba serikali inatimiza majukumu na ahadi zake kwa watu wa sehemu hizo. Mjumbe mmoja mmoja wa Baraza anaweza kufanya uangalizi kwa kupitia na kuchukua hatua kwa maovu yanayofanywa na Serikali kuu na Serikali za mitaa katika jimbo lake.

## 4.3 Mahakama

Kazi ya msingi ya mahakama ni kutafsiri sheria, uendeshaji wa kesi, na utoaji wa haki kwa mujibu wa sheria za nchi. Kutokana na hayo mahakama ina majukumu mawili muhimu katika utawala bora.
Kwanza mahakama imepewa mamlaka ya kuamua kesi za madai na jinai na kwa hivyo ni taasisis muhimu sana katika kukuza utawala wa sheria na haki za binaadamu, ambayo ni moja ya msingi wa utawala bora. Pili, mahakama yenyewe inapaswa kuheshimu misingi ya utawala bora wakati wa utekelezaji wa majukumu yake na shughuli za ofisi.

### 4.4 Taasisi za Uangalizi

Taasisi za uangalizi zina majukumu muhimu sana ya kuhakikisha kwamba misingi ya utawala bora inafuatwa.

#### 4.4.1 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Jukumu la ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni kuhakikisha kunakuwa na nidhamu katika matumizi ya Serikali. Ofisi inakagua hesabu zote za wizara, idara, na taasisi za serikali. Ukaguzi unafanywa kwa ajili ya kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji na ugawaji wa raslimali za umma ili kuchangia maendeleo endelevu kijamii na kiuchumi.

#### 4.4.2 Kamisheni ya Utumishi wa Umma (PSC)

Kamisheni ya Utumishi wa umma iliyoazishwa hivi karibuni ina kazi ya kuuangalia Utumishi wa Umma na masuala yote ya usimamizi wa rasilimali watu hasa yanayohusiana na ajira. Hii ni sehemu muhimu ya uangalizi na uwajibikaji kwa waajiriwa wa Serikali.

#### 4.4.3 Mamlaka za Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi.

Mamlaka ya kupambana na rushwa na ile ya kusimamia Maadili ya Viongozi zinajukumu kubwa la kuzuia rushwa katika sekta za umma na binafsi; katika kuchunguza na kuendesha mashitaka kwa matukio yote ya rushwa; katika kusimamia na kuendeleza maadili ya viongozi, na kutoa muamko miongoni mwa wananchi wa Zanzibar juu ya aina na madhara ya rushwa. Mswaada wa sheria ya kuzuia rushwa utatayarishwa ambao utaanzisha mamlaka huru ya kuzuia rushwa na ule wa kusimamia maadili ya Viongozi pia utatayarishwa ambao utaanzisha mamlaka ya Kusimamia Maadili ya Viongozi.

#### 4.4.4 Vyombo vya habari

Zanzibar kuna vyombo vya habari vya umma na binafsi (Magazeti, majarida ya wiki, redio, televisheni na intaneti). Katika miaka ya karibuni vyombo vya habari vimekuwa vikipewa uhuru zaidi. Majukumu ya vyombo vya habari ni kutoa habari kwa umma na kuwa kama chombo cha

uangalizi. Vyombo vya habari vya umma na vile vya binafsi vinajukumu kitaaluma la kuipasha habari jamii katika mambo muhimu, sera, sheria, na kuendesha kampeni za wazi ambazo ni sehemu ya ajenda za utawala bora. Vyombo vya habari pia vimepewa kazi ya kuitathimini Serikali katika utendaji wake na kuripoti juu ya uongozi mbaya, ukiukwaji wa majukumu, rushwa au aina nyingine ya uongozi mbaya.

### 4.4.5 Jumuiya za Kiraia

Jukumu la Jumuiya za kiraia kwa upande mmoja ni mbia wa serikali katika kuunda sera na kutayarisha mipango ya utekelezaji kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya Wazanzibari. Kwa upande mwingine, taasisi Zisizo za kiserikali pia zipo kwa ajili ya kutathmini matendo ya Serikali na athari zake katika utowaji wa huduma na ikiwezekana kuelezea shida zao. Zaidi ya hayo, Jumuiya za kiraia hazina budi kuheshimu misingi ya utawala bora wakati wa kutekeleza shughuli zao kama zilivyowekwa na taasisi ya kimataifa ya viwango (ISO) 26000.

### 4.4.6 Sekta Binafsi

Sekta binafsi zinajulikana kama ni mshirika wa maendeleo na ni mtoaji mkuu wa bidhaa na huduma kwa jamii. Serikali inatambua kuwa biashara ni kiungo muhimu katika ukuaji wa uchumi na kwamba ubia baina ya taasisi za umma na zile binafsi ni muhimu. Ili kuhakikisha kwamba utwala bora unaimarika hapa Zanzibar, sekta binafsi lazima ibebe majukumu la kukuza utamaduni wa kupambana na rushwa, kuimarisha uwazi na tija katika kufunga mikataba, kutoa tenda, ushuru na leseni. Watendaji wa sekta binafsi lazima wafanye kazi na serikali katika kuweka mifumo ya kuzuia watu wachache kuhodhi biashara na kuwanyonya wateja, pamoja na kufanya kazi na serikali katika kuazisha sera juu ya ubia wa taasisi za binafsi na zile za umma. Ni muhimu kwa taasisi za biashara za ndani na za kimataifa kuweka maadili ya utendaji na taratibu za kutoa ripoti kwa mujibu wa viwango vya kimataifa. Mifumo na misingi hii inaweza kuzisaidia jamii ya wafanya biashara wa Zanzibar kutekeleza misingi ya utawala bora na zaidi kuweza kishindana katika viwango vya kikanda na kimataifa.

### 4.4.7 Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) na Taasisi za kidini

Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) na taasisi za kidini zinaweza kutoa uangalizi kwa serikali kuu, serikali za mitaa, na sekta binafsi. NGOs na taasisi za kidini pia zitashajiisha makundi tafauti katika jamii, hasa katika kuondoa maovu kama vile rushwa na kutotendewa haki. NGOs na taasisi za kidini zinaweza kutoa sauti kwa makundi tafauti kuhusu maamuzi ya kisiasa na ya serikali na kuelimisha umma kuhusu masuala ya kiutawala. Jumuiya na taasisi hazina budi kushirikishwa kikamilifu katika taratibu za kuunda sera. Serikali lazima wakati huo huo ijikite katika kuziongoza na kuzielewesha NGOs na Taasisi za kidini faida ya kuheshimu misingi ya utawala bora wakati wa kutekeleza kazi zao.

### 4.4.8 Washirika wa Maendeleo.

Washirika wa maendeleo ni wadau muhimu katika utawala bora. Washirika hao wanasaidia juhudi za Serikali katika miradi kadhaa ya maendeleo kwa kutoa misaada ya fedha na ya kiufundi. Katika utawala bora washiriki wa maendeleo wanaimarisha ufanisi wa misaada na wanafanyakazi kwa karibu sana na serikali katika kutafuta fedha na misaada ya kiufundi. Wakati huo huo, washiriki wa maendeleo wenyewe binafsi wanapaswa kufuata mising ya utawala bora wakati wa kutekeleza shughuli zao hapa Zanzibar. Wakati washirika hao wa maendeleo wanazo kanuni zao za maadili na mambo yanayolingana na hayo, sio wote wenye vyombo hivyo na hata wale wenye vyombo hivyo uelewa wao kwa vyombo hivyo sio mzuri kama unavyotakiwa.

## 5.0 MUUNDO WA UTEKELEZAJI WA SERA

### 5.1 Utekelezaji wa Sera

Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na (KKUB) itaratibu utekelezaji wa sera hii wakat wizara, idara, na taasisi zote za Serikali zitakuwa na jukumu la pamoja kwa utawala bora hapa Zanzibar. Taasisi za uangalizi na Jumuiya za kiraia zitakuwa na jukumu la pamoja la kuwezesha utekelezaji wa sera hii.

### 5.2 Marekibisho ya Sera

Serikali inaweza kubadilisha sera hii kwa lengo la kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea katika mazingira ya utawala bora ili kuwezesha utekelezaji wake.

### 5.3 Ufuatiliaji na Tathimini

Wizara inayoshughulikia utawala bora kwa kusaidiana na (KKUB) itatayarisha muundo wa ufuatiliaji na tathimini kwa utekelezaji wa sera hii. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yataingizwa katika ripoti ya mwaka ya utawala bora ya Zanzibar.